# Ukombozi Reloaded



Shemeji Melayeki

UKOMBOZI RELOADED ©2018 Shemeji Melayeki

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi isipokuwa kwa nukuu mbalimbali na matumizi ya kufundishia.

SIMU: +255 714 548 565/+255 763 965 297
Email: shemeji.melayeki@gmail.com
YouTube: Shemeji Melayeki
Instagram: apostle_shemeji_melayeki
Twitter: @melayeki
Facebook: Ap Shemeji Melayeki

Kimepigwa chapa na: CLIMAX SOLUTIONS – ARUSHA
+255 (0) 658 288 054
+255 (0) 687 699 862
+255 (0) 763 965 297
climaxsolutions8@gmail.com

YALIYOMO

Utangulizi........................................................................ 1

Ukombozi ni nini hasa? ................................................................ 4

Ukombozi unapatikanaje?.............................................. 6

Ukiokoka unahitaji kukombolewa? ................................ 8

Hakuna Ukombozi nje ya Yesu .................................... 10

Laana za ukoo na vifungo ............................................ 12

Maombi ya Ukombozi ................................................. 14

Kwa hiyo umeokoka? .................................................. 16

Wokovu ni nini?........................................................... 20

Tatizo lilikuwa wapi?.................................................... 25

Kwanini Afrika?........................................................... 31

Uongo na matokeo ....................................................... 32

Kiumbe kipya............................................................... 34

# Utangulizi

Mwanzoni Mwa mwaka 2018 nilianza kufuatilia kwa upya masomo yahusuyo ukombozi (deliverance/redemption) na kuna baadhi ya mambo Roho Mtakatifu alikuwa ameanza kunifundisha... katika kitabu hiki nitatoa baadhi ya mambo niliyojifunza.

Soma: Waefeso 1:3-7 [3] Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo; [4]kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. [5]Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. [6]Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa. [7]Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.

Niliposoma hapa, nikashtuka kuona haya:-

1. Katika Yesu Kristo (ndani ya Yesu) kuna Baraka zote za Rohoni (laana haipo) kwa mtu aliye ndani ya Yesu Kristo.

2. Alituchagua tuwe watakatifu (hatukujifanya watakatifu) yaani ili tusiwe na hatia mbele zake. (HII KAZI AMEFANYA YEYE) (Wakati uliopita).

3. Kwa njia ya Yesu Kristo tunafanywa wana wa Mungu kwa hiyo Yesu alituhamisha ukoo tukawa uzao wa Mungu halafu ni kwa mapenzi yake tena (hapa laana za ukoo wa Mungu Baba kama zipo ndiyo zinatakiwa zinifuate kwa sababu nimehamia huo ukoo kwa kumpokea Yesu Kristo badala yake kuna BARAKA)

4. Tunaisifu Neema yake (yaani siyo nguvu zetu wala sadaka zetu wala maombi wala mafungo yetu) yametuneemesha KATIKA huyo Mpendwa (herufi M kubwa yaani Yesu).

5. Katika Mpendwa huyo (Yesu Kristo) TUNAO UKOMBOZI, MASAMAHA YA DHAMBI SAWA SAWA NA WINGI WA NEEMA YAKE.

Tena Yesu alimaliza hiyo kazi kabisa.. Wakolosai 2:13-15
[13]Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote;
[14]akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani;

[15]akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo.

## Ukombozi ni nini hasa?

1 Timotheo 2:5-6 [5] Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; [6]ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake.

Neno la Kiingereza lililotumika pale kama Ukombozi ni Ransom kwa Kigiriki ni antilutron.

Meaning: What is given in exchange for another as the price of his redemption.

Kiswahili: Kilichotolewa kwa ajili ya kukikomboa kingine (kama malipo). Baada ya kusoma hapa nikapigwa na mshangao tena....

Unajua nilishangaa nini?

1. Mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja (Yesu) hakuna sadaka ya upatanisho zaidi yake.

2. Na kwenye upatanisho huo kwa sababu kulikuwa na tatizo Yesu aliamua kuwa sadaka ya Ukombozi ili kukomboa uhusiano uliopotea kati ya Mungu na wanadamu kwa mwanadamu kuuzwa chini ya utumwa wa dhambi. Mungu hakukasirikii kwa kuwa babu yako alikuwa mganga

wa kienyeji au mchawi au alikuwa ameua watu 200 na kujenga madhababu ya ukoo. Kuangamia kwako ni matokeo ya kukataa ushirika huu kwa njia ya mwanae ambaye ametupatanisha.

Wewe na Mungu Baba mmepatana kwa njia ya Yesu Kristo...Mambo ya babu yako atajaza mwenyewe kwa nafasi yake ikiwa HAKUAMINI.

Ikiwa haujampokea Yesu Kristo moyoni mwako hii haikuhusu, kumpokea Yesu ni kupokea ukombozi wake. Ni kukubali kuwa mali ya Mungu ni kukubali kuwa pamoja na Baba akupendaye.

# Ukombozi unapatikanaje?

Wakolosai 1:13-14 [13] Naye alituokoa (wakati uliopita) katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; (ukiwa hapa ndiyo umeokoka) [14] ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;

Kwa King James Version IMEANDIKWA

13 [For He] has delivered us from the power of darkness and has translated [us] into the kingdom of His dear Son; 14 in whom we have redemption through His blood, the remission of sins.

Naomba uangalie haya maandiko... Neno alituokoa - has delivered us limetumika kama rhuomai lina maana hii to draw to one's self, to rescue yaani kuokoa kutoka sehemu nyingine na kujiletea (gizani kuja kwa Yesu). Kwenye neno hili delivered ndipo tunapopata neno DELIVERANCE. Kwa muktadha huu DELIVERANCE ni matokeo ya REDEMPTION. Yaani tumeokolewa (delivered) kwa sababu ya malipo yaliyoafanyika (redemption) na Yesu Kristo ambapo msamaha wa dhambi umeshatolewa.

Najiuliza ni nani anayewarudisha watu waliookoka kule? Kiasi kwamba inabidi tuwakomboe tena?

Mstari wa 14 neno ukombozi yaani redemption nimetumika kama apolutrōsis.

Maana yake:

° Releasing effected by payment of ransom

°Liberation procured by the payment of a ransom

Yaani kuwekwa huru kutokana na deni lililolipwa, au kilichotolewa mbadala.

Bado watu waliookoka wanaambiwa wana vifungo kadha kadha wa kadha ambazo Yesu Kristo hakuzishughulikia. Hivi kuna maombi yanaweza kuvunja kile ambacho Yesu hakukivunja?

Jifunze kupokea neema ya Mungu na kile alichokifanya Yesu msalabani.

NB: Ukombozi hauombwi ila unapokelewa na Mtu aliyejua ya kuwa Yesu Kristo alilipa msalabani deni lake lote.

Namna bora ya kukombolewa ni kuamini na kukiri alichokifanya Yesu msalabani! Kuna watu wanaimba "Dhambi zangu zote wala si nusu zimewekwa msalabani, wala sichukui laana yake ni salama rohoni mwangu" halafu wakitoka kanisani wanapinga walichokiimba.

# Ukiokoka unahitaji kukombolewa?

Ngoja niseme kama risiti za maduka ya wahindi "Mali iliyonunuliwa hairudishwi yaani GOODS ONCE SOLD CANNOT BE RETURNED".

Wafilipi 2:8 [8] tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.

Lengo lake kunyenyekea hadi mauti ya msalaba ni ili atununue sisi tuliokuwa tumeuzwa na kustahilishwa mambo yasiyokuwa mpango wa Mungu Baba yetu wa Mbinguni.

Kwenye kitabu cha Ufunuo wa Yohana jopo lililosimama mbele ya kiti cha enzi walianza kumsifia Mwanakondoo (Yesu) kwa sababu ya kile alichokifanya. Angalia walichosema;

Ufunuo wa Yohana 5:8-10 [8] Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu. [9] Nao waimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa,

ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, [10] ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi.

Ukweli kuhusu wewe ni nani ndani ya Kristo ni hii; umenunuliwa kwa damu ya thamani ya gharama kubwa ya Yesu Kristo (kufa kwake) kutoka kwenye kabila lako, lugha, jamaa na taifa ili uwe aina nyingine ya mtu ambayo unaitwa Mwana wa Mungu, kwenye ufalme wa Mungu, taifa la Mungu na raia wa Mbinguni

Tena Petro anasema,

1 Petro 2:9-10 [9] Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; [10]ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema.

Mtu yeyote akikupa tafsiri ya Wewe ni nani kama inakinzana na kile Neno la Mungu linasema juu yako wala haitambua kazi aliyofanya Yesu pale msalabani Kamwe USIKUBALI kwani kufanya hivyo ni KUIDHALILISHA KAZI YA MSALABA WA YESU.

Kazi ambayo hakuna mtu mwingine awezaye kufanya.

# Hakuna Ukombozi nje ya Yesu

Wakati nikiwa mlimani Duluti mtumishi mmoja alinifuata akaniambia "Mtumishi wa Mungu Shemeji" nikasema "Naam" akasema "Najitahidi kumfundisha Yesu nashindwa kabisa, mimi natafuta tu mistari ya Agano la Kale yanayozungumzia vifungo, sasa ukimhubiri Yesu sana unaona uhuru huoni vifungo. Sasa hii sioni zile amsha amsha za watu kudondoka kulia n.k"

Nikashtuka sana kusikia hili jambo. Nikamwambia "Sijui kwanini umeniuliza lakini Ndiyo somo ninalofundisha sasa Hivi mtandaoni"

Nikaongea naye muda mrefu sana. Akasema "Tatizo langu nina miaka saba nafundisha haya mambo na kuendesha maombi mazito sana hivyo siyo rahisi mimi kuyaacha"

Uongo maarufu ni uongo tu!

Nikaendelea kumfundisha huku wengine wakisikiliza kwa makini.

Baada ya kunyamaza hali ya hewa ikabadilika, wale wengine wakaanza fujo isiyokuwa ya kawaida. Nikawaambia "KAMA INAWAUMA JIULIZENI KWANINI"

Nikaongeza "mfunueni kristo halisi na watu watawekwa huru, kinyume na hapo mtawafunga watu kisaikolojia na kujifanya mnawafungua kwa maombi"

Nikawaambia "Kwa nini mnawaita watu kwenye majukwaa ya nje mkiwaambiwa Njooni kwa Yesu ili muwe HURU wakifika kwenye Semina za ndani mnawaambia Bado hamko HURU?

Wakanikasirikia zaidi. Hii ni kuonyesha ya kwamba watu wengi hufungwa zaidi na mafundisho kuliko kufunguliwa. Badala ya kuwafundisha watu kile walichokipokea katika Kristo wanaanza kudokoa mistari ya Agano la Kale na kuyasoma nje ya muktadha ili mradi wawanase watu kwa hofu na baadaye kuanza kuwafungua tena. Ndiyo maana watu wanaoanguka ni wale wale kila wakati wala kile wanachokiita “kifungo” hakiwaachii.

# Laana za ukoo na vifungo

Angalia 2 Wakorintho 5:17 [17] Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.

Ni nani anayesadiki hili, uko ndani au nje ya Kristo kwa sababu hiyo ndiyo inayoamua kwamba wewe ni Mpya au wa zamani. Ukiingia ndani ya Yesu unakuwa totally disconnected na maisha yako ya zamani (asili yako ya dhambi). Cha Muhimu hapa ni kujifunza kuuishi upya wa maisha yaliyopo ndani ya Kristo Yesu na kujua kwa hakika nini kilichotokea ili kuishi sawa sawa na wokovu uliyoletwa na Kristo Yesu. Hii ndiyo inatakiwa kuwa kiu kubwa ya watu waliozaliwa upya (Born Again) na ndiyo lengo la UANAFUNZI.

Maombi ya kujitoa makaburini, kukomboa vitovu, kuvunja maneno ya wazee, kukomboa nyayo, kujitoa kwa waganga, kufungua vifundo, kurudisha nafsi zilizoibiwa ni kuiga taratibu za kichawi ambayo si Bwana wetu Yesu Kristo wala Mtume Paulo au hata basi Petro au Yakobo wala Yohana aliyewahi kufundisha haya. Ndugu zangu, tutafute yaliyo juu ambapo Kristo Yesu yupo.

Tuache kuumiza hisia za watu na kujiumiza. Kwani ni wangapi kati yetu wanajua vitovu vyao vilipo, au tukienda saluni tuwe tunaondoka na nywele zetu? Na kama tumeibiwa nafsi tunapate uelewa wa kile tunaambia na wakati akili iko kwenye nafsi? Je, haifai hata kutumia akili kidogo na kuona kwama tunaendekeza uganga kwa jina la Yesu?.

Yesu ndiye ukombozi wetu, tumjue Yeye. Kuwajua wachawi, Freemason, waganga, majini na mambo yafananayo na hayo ni sumu sana (hakuna mema yoyote yatokanayo na kujua hayo) huku wakristo wengi wakiwa hawamjui kabisa Yesu na sababu yake ya kuja kwetu. Mtu anapita fellowship na kugawa vipeperushi vya freemason au illuminati badala ya kusambaza injili ya Yesu kwa kasi.

# Maombi ya Ukombozi

Ukombozi (Redemption) ilifanyika msalabani na wakati huo hakuna mwanadamu aliyeanzisha ila ni Mungu mwenyewe kwa sababu mwanadamu alipotea na hakuwa na Mungu akaona namna bora ya kumsaidia ni kutafuta mwanakondoo (Yesu Kristo) achinjwe ili alete ukombozi wa Mwanadamu. Mwanadamu akiupokea huu ukombozi (ransom) anakuwa ameokoka (Saved/Delivered) kutokana na uharibifu uliopo na ujao. Ndiyo maana Wokovu ni uhakika wa maisha ya sasa na ya baadaye (present to eternity).

Hivyo basi Kukemea mapepo siyo ukombozi ni matunda ya Ukombozi.

Kwamba hayana uhalali tena wa kuyaongoza maisha ya mwamini wala kuyatawala kwa sababu alishanunuliwa na hana madai yoyote tena ndani yake. Ndiyo maana tunayo mamlaka hayo kwa sababu ya kazi ya Ukombozi ulio katika Kristo Yesu.

Tatizo ni hili, wengi hatujui hili, Wagalatia 2:20 [20] Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.

Hii ndiyo salama yetu, ni Kristo ndani yetu!..

Kuokoka siyo Kumkiri Yesu, Kumkiri Yesu ni ishara ya kwamba unaamini kazi aliyofanya kwa ajili yako.. hivyo kusema Nimeokoka halafu hujui umeokoka kwenye lipi ndiyo shida ya watu wengi! Hebu jiulize unavyoambiwa umeokoka umewahi kufikiri hatari ilikuwa ni nini? Mbona wakristo wengi kama bado wanaambiwa wako hatarini?

Hatari dhidi ya wachawi, mapepo, laana, hatari dhidi ya Mungu mwenyewe na hata moto wa Jehanamu!? Sasa umeokoka kutoka kwenye nini?

Waingereza wangesema; Hey, Relax! You're Saved. You're out of danger!

## Kwa hiyo umeokoka?

Watu wengi wanaosema "wameokoka" aidha wamesingiziwa kuwa wameokoka au wanajidanganya wameokoka au hawajaambiwa "KWELI" kwamba wameokoka kutoka kwenye nini ama ile sala waliyoongozwa pengine ndiyo wanafikiri ni wokovu!.

Haya yote yanahitaji shule zaidi lakini nitasema mambo kadhaa katika mtiririko huu!

Kwa kutokujua hili wamekuwa victims wa vitu vya ajabu na huku wakifanya "Wokovu" uonekane ni Dini tu au mtindo wa kuitana unaotokana na kuwa au kuhamia "dhehebu" fulani. Ndiyo maana kuna baadhi ya watu wanakuuliza "Umeokoka? Ukisema ndiyo, wanaongeza "Unasali wapi?" Ukijibu dhehebu fulani watakuambia aidha hujaokoka "vizuri" au hamia dhehebu letu ili uokoke vizuri.

Hawa pia wamechangia kabisa kuharibu maana ya wokovu...

NB: Hakuna uhusiano wowote wa wokovu na madhehebu fulani fulani.

Ukiupokea Ukombozi wa Yesu (aliofanya kwa ajili yetu msalabani) unakubali na kuamini unaishi maisha yasiyo na hofu tena, maisha yaliyo juu zaidi.

Kuokoka ni kwamba uko salama mtu asikuambie unatakiwa uongezee bla bla bla ili uwe salama zaidi (hao ndio wanamrudishia Yesu msalabani kwa kudharau kazi kubwa aliyoifanya).

Watu wengi hawajui kabisa hii maana ya wokovu. Wengine hawajui kabisa wameokoka kutoka kwenye nini.... na sasa hivi wako kwenye nini? Siku hizi kila mtu anasema ameokoka na anaishi kwenye hofu ya mambo lukuki - yaliyopita, yaliyopo na yajayo. Ndiyo maana usidanganyike tu kwa mtu kukuambia nimeokoka au nimeamini. Muulize, "Unaamini nini?"

Imagine unamuuliza mtu "Umeokoka?" Anakujibu "Ndiyo"

Ukizunguka ukamuuliza "Kwa hiyo utaenda mbinguni?"

Hapo kwanza anasita na anakula kamuda akiwazaaa ... Baadaye anakujibu "Sina uhakika" mwingine akanijibu "inategemea"

Nikauliza "Inategemea nini?"... Asilimia kubwa wakajibu "Inategemea watakufa wakati gani, yaani kabla ya kukata roho unatubu"

Nikauliza sasa "Ukiwa unasoma text ya rafiki yako ukiwa ndani ya daladala huku hujaanza kutubu ghafla kama

Akwilina (MWANAFUNZI aliyepigwa risasi akiwa kwenye daladala) risasi ikapita kichwani paaah hauendi mbinguni!?"

Akakaa, Kimya!.....

Nikauliza "Uliposema Umeokoka, Je, Umeokoka kutokana na nini?"

"Kama mbinguni unaingia kwa matendo yako, kwa nini sasa Yesu ALIKUFA? Kama unahisi kwenda mbinguni 'it depends on you' sasa Yesu wa kazi gani?"

Angalia Paulo alivyoandika… kwenye Tito 3:4-7
[4]Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa;
[5]si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;
[6]ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu;
[7]ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu.

Angalia haya maneno *"si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali"*
Waefeso 2:8-9
[8]Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu;
[9]wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.

Tena alirudia na hapa *“wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.”*

## Wokovu ni nini?

Hii inatuonyesha kuwa watu wengi sana hawajui wala hawaelewi maana ya wokovu.

Watu wengi wanaweza kuongozwa Sala ile ya "Mimi ni mwenye dhambi .........Na kuendelea" lakini wasijue hakika ni nini wanachokifanya.

Kukiri siyo Muhimu sana kama huamini moyoni. Kuamini ni matokeo ya taarifa sahihi....

Kama ulivyoandikwa kwenye, Warumi 10:9-10 [9]Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. (Future tense) [10]Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.

Na neno hili hapo juu halifundishi kuungama dhambi bali kukubali na kuamini kwamba Yesu ni Bwana pamoja na Ufufuo wake. From Cross to Resurrection na kwamba unaamini ya kwamba kwa kufa kwake dhambi zako zimeondolewa na kwa kufufuka kwake umehesabiwa haki. Lakini pia, neno kukiri/confess bila kuamini moyoni isingekuwa na maana kabisa kwani nafasi ya mabubu, viziwi

kusingekuwepo ndiyo maana neno la Kigiriki pale ni Homologeō homo (uniform au moja) na logeo ni neno kwa hiyo ni in agreement in what has been said or done yaani kukubaliana na kile Yesu Kristo AMEFANYA kwa ajili yako. Kwa hiyo hata bubu, kiziwi anaweza kuokoka (They can agree). Kuokoka ni zaidi ya kuongozwa Sala ya toba. Mtu anaweza kukiri mdomo bila kuamini moyoni.

Angalia Jinsi Yesu na Mwizi msalabani walivyomaliza, yule mwizi aliamini na akaponea pale pale. Sasa concept ya wokovu ni tatizo zaidi.

Kwenye Warumi 10:10 neno wokovu limetumika neno la Kigiriki, sōtēria. Maana yake…

1. Deliverance, preservation, safety! (Ukombozi, kuhifadhiwa, kuwa salama). Kuambiwa umeokoka unatakiwa kufanyiwa deliverance ni hatari.

2. Deliverance from the molestation of enemies (Kukombolewa kutokana na mateso ya maadui)

3. Salvation as the present possession of all true Christians (Wokovu kama Haki (kumiliki) kwa wakristo wa kweli

4. The sum of benefits and blessings which the Christians, redeemed from all earthly ills, will enjoy after the visible return of Christ from heaven in the consummated and eternal

kingdom of God. (Jumla ya faida na baraka zote ambazo wakristo waliokombolewa kwenye mateso ya dunia watafurahia kristo atakaporudi na katika ufalme wa Mungu wa milele).

Mambo yafuatayo yapo kwenye tafsiri hiyo.

KUKOMBOLEWA KUTOKANA NA MAMBO YALIYOPITA, KUWEKWA SALAMA KWA AJILI YA YALE YALIYOPO NA maisha ya MILELE wa BAADAYE. This is a full size package. Past, Present and Future.

Tafsiri ya kwanza ndiyo inaonyesha kuwa ukombozi siyo maombi ni matokeo ya Salvation/Wokovu. Sasa ukiambiwa umeokoka unaelewa unachoambiwa. UKO SALAMA KWA YALIYOPITA, YALIYOPO NA YAJAYO.

Huu ukombozi unaitwa UKOMBOZI WA MILELE.. angalia mwandishi wa Waebrania anavyoelekea Waebrania 9:11-14
[11]Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu,
[12]wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele.

[13]Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili;
[14]basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?

Damu ya mbuzi na wanyama ilikuwa inaruhusu kumbukumbu la dhambi kila baada ya mwaka ila damu ya Yesu inafuta na kuondoa kabisa makosa. Hii ni sawa na kusema inasafisha milele.

Waebrania 10:1-4
[1]Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao.
[2]Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi?
[3]Lakini katika dhabihu hizo liko kumbukumbu la dhambi kila mwaka.
[4]Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.

Ndiyo maana aliahidi kuwa HATAZIKUMBUKA TENA…
Waebrania 8:12
[12]Kwa sababu nitawasamehe maovu yao,

Na dhambi zao sitazikumbuka tena.

Akarudia tena hapa…
Waebrania 10:14-18
[14]Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.
[15]Na Roho Mtakatifu naye amshuhudia; kwa maana, baada ya kusema,
[16]Hili ni agano nitakaloagana nao baada ya siku zile, anena Bwana,
Nitatia sheria zangu mioyoni mwao,
Na katika nia zao nitaziandika;
ndipo anenapo,
[17]Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa.
[18]Basi, ondoleo la hayo likiwapo, hapana toleo tena kwa ajili ya dhambi.

Angalia haya maneno *Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.* Tena asema KWA TOLEO MOJA si la kila siku.

## Tatizo liko wapi?

Tangu 2004 nilipoanza kufundisha neno la Mungu, niliona watu wengi wanaofundisha "False Deliverance" wanatumia Yohana 11:44 [44] Akatoka nje yule aliyekufa, amefungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake amefungwa leso. Naye Yesu akawaambia, Mfungueni, mkamwache aende zake. Wanasahau mistsri yote aliyoyasema Paulo na kuanza kutengeneza mafunuo yao binafsi sehemu ambayo hata neno UKOMBOZI haujatajwa.

Mpaka leo hii bado inatumika. Kama mstari wa kuwahakikishia kuwa kila aliyeokoka ana vifungo.

Hii ni kuchukua maandiko nje ya muktadha, kwa sababu:-

1. Wako watu wengi wamefufuliwa na Yesu inakuwaje tu ya Lazaro yenye sanda ihusishwe na deliverance?

Wale wengine waliofufuka hawakuwa na vifungo? Kimya!

2. Kama tunafananisha kufa na kufufuka kama wokovu (sasa wale wengine waliofufuka na Yesu hakusema mfungueni hao hawakuwa na vifungo?)

Lazaro alikuwa kaburini na asingeweza kufungua sanda alizofungwa huna haja ya kujitahidi kurohoisha iko wazi, Yesu alimaanisha nguo alizofungwa. FULL STOP. Somo kubwa ambalo tunaona Yesu alitaka watu wajifunze pale ni

kwamba Yeye ndiye ufufuo na uzima, angalia Yohana 11:21-27

[21]Basi Martha akamwambia Yesu, Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa.

[22]Lakini hata sasa najua ya kuwa yo yote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa.

[23]Yesu akamwambia, Ndugu yako atafufuka.

[24]Martha akamwambia, Najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho.

**[25]Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi;**

**[26]naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je! Unayasadiki hayo?**

[27]Akamwambia, Naam, Bwana, mimi nimesadiki ya kwamba wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, yule ajaye ulimwenguni.

Kitu kingine kinachotumika ni Maombolezo 5:7 [7]Baba zetu walitenda dhambi hata hawako; Na sisi tumeyachukua maovu yao.

Haya ni maombolezo ya Yeremia baada ya wazee kufanya makosa na watoto wakajikuta wako utumwani. Wala siyo laana za ukoo ni maamuzi mabaya ya wazee. Mbali na hayo tu kwa maana ya mtu kurithi uovu wa baba yake Ezekieli alitabiri vizuri tu hebu soma Ezekieli 18:1-4 [1]Neno la BWANA likanijia tena, kusema, [2]Je! Maana yake ni nini hata mkatumia mithali hii katika Israeli, mkisema, Baba wamekula zabibu mbichi, nao watoto wakatiwa ganzi la meno? [3]Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, hamtakuwa na sababu ya kuitumia tena mithali hii katika Israeli. [4]Tazama, roho zote ni mali yangu; kama vile roho ya baba ni mali yangu, ndivyo ilivyo roho ya mwana mali yangu; roho ile itendayo dhambi itakufa.

Sasa kama Mungu mwenyewe amekataa Kwanini bado wanang'ang'ana na kuvunja generational curses?"

Sehemu nyingine ni Kutoka Kutoka 20:5-6

[5]Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, [6]nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

Kama mtu akikusomea haraka mstari wa 5 unaweza kuanza kumuwaza babu yake aliyekuwa anaabudu chini ya mti na

kutoa sadaka. Wengi huwa hawasaomi mstari wa 6 kwa sababu lengo lao ni kukulazimishia ujione umelaaniwa. Jambo muhimu la kuona hapa ni kwamba UKIWA MWAMINI, WEWE SI KIZAZI KUMCHUKIZACHO MUNGU. WEWE NI MWANA WA MUNGU TENA UPENDWAYE NA BABA. MUNGU AMEKUPA REHEMA WALA SI CHOCHOTE KILE.

Kusema nawarehemu maelfu elfu siyo idadi ya watu ila idadi ya vizazi kwenye Amplified Bible wanatumia thousands generations that loves God and keep His commandments.
Angalia Exodus 20:6 [6]But showing mercy and steadfast love to a thousand generations of those who love Me and keep My commandments.

Jumla ya amri zote za Mungu ni Upendo. Mungu alitupenda kwanza na sisi tumempenda na ndiyo maana tumeamini. Tumeukubali upendo wake. Ametupa namna ya kupenda na sisi tunawapenda wengine pia. 1 Yohana 3:23 [23]Na hii ndiyo amri yake, kwamba tuliamini jina la Mwana wake Yesu Kristo, na kupendana sisi kwa sisi, kama alivyotupa amri. Tena Yohana anasema 1 Yohana 4:19 [19]Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza. 1 Yohana 4:21

[21]Na amri hii tumepewa na yeye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake.

Tumeamini na 1 Yohana 5:1-3

[1]Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu. Na kila mtu ampendaye mwenye kuzaa, ampenda hata yeye aliyezaliwa na yeye. [2]Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. [3]Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito.

AMRI ZAKE SI NZITO KWA SABABU UPENDO UMEMWAGWA NDANI YETU KWA ROHO WA MUNGU TULIYEPEWA. (WARUMI 5:5) ndiyo maana upendo ni tunda la Roho. Hii ina maana tunayo chemchemi ya upendo. Amri zake si nzito.

Lengo langu lilikuwa ni kuwafanya WAKRISTO wawe Active wanaposoma na kusikiliza neno la Mungu kwa sababu mambo mengi yamechakachuliwa na yanazidi kuchakachuliwa.

TUSIWE KAMA MAKINDA KUPOKEA NA KUMEZA, TOA WALI, TEMA MAWE! Hata kama ulilishwa na mheshimiwa mtume wa mitume wakuu Shemeji Melayeki una haki ya kuPIMA. Kila mtu ana Haki ya kukosea hata kama Dunia nzima inamwinamia.

Wakristo wamefundishwa nidhamu ya uoga kwa kasi sana kiasi kwamba hata walifundishwa uongo hawasemi wala kuchunguza maandiko kama watu wa Beroya! Pamoja na miujiza mikubwa aliyoyafanya Bwana kwa mkono wa Paulo lakini watu wale bado waliyapitia maandiko kuona kama ndivyo ilivyo au wametia chumvi. Lakini pia tuone UPENDO wa Mungu usio wa kawaida jinsi alivyotukomboa hata wakati hatujui kuwa tumeuzwa!

# Kwa nini Afrika?

Mtu mmoja aliniambia "Nimechunguza makanisa mengi ya Ulaya na Marekani, haya mambo ya laana za ukoo na Maswali ya uganga, Uchawi, kukomboa nyayo, kukomboa vitovu n.k, havipo" nikamjibu "Kule wana mambo yao lakini pia huku tumeathiriwa na tamaduni zilizokuwepo"

The gospel has been Africanized yaani mambo yetu ya kichawi tumehamishiwa kanisani. Watu wakienda kwa mganga lazima upewe kitu cha kushikilia, mambo yakibuma unakimbilia hicho kitu na mambo yanayofanana na hayo. Na sisi tunataka tukienda kanisani, tupewe vitu vya kushikilia, Mtoto akiumwa ukimbilie mafuta, chumvi, maji, fruto, leso, mawe, sabuni, n.k hapo unaunganisha kidogo na jina la Yesu Kristo inaonekana imefanyika ki-YesuYesu.

Hata tukiambiwa umeokoka unatafuta ishara au kitu kinachoshikika cha kukuonyesha kuwa umeokoka!

Mtu mmoja alisema "Yaani hata nimeombewa lakini sijaanguka, Hivi Nimeokoka kweli?"

Petro wakati anahutubia mkutano akasema Matendo ya Mitume 2:21 [21] Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa.

## Uongo na matokeo

Siku moja nikiwa kwenye kanisa kubwa lenye maelfu ya waumini, MCHUNGAJI alianza kufundisha jambo linakinzana na ukweli wa neno la Mungu. Kwenye moyo wangu ikaanza kugoma 'Hii haiko sawa' nikajiambia "Wewe uliwahi kukusanya watu wengi kiasi hiki?" Nikajijibu "Hapana" likaja swali la Pili "Wewe una gari Kali kama la mtumishi?" Nikajijibu "Hapana" Kama vile nazinduka usingizini nikasikia sauti nyingine ikinihoji;Akaanza kwa kusema "Mwaka 2001 ukiwa kidato cha kwanza kwenye mtihani wa Annual Physics ulipata 98%" nikasema "enheeee"; "Lakini ulidanganya" nikawahi "Kivipi?" Nikauliza "Swali la Topic ya Density ambalo liko kwenye TIE book 1 la mwisho jibu ni 921 (swali la Alloy)"

Nikaendelea kusikiliza "Tangu ufundishwe hukuwahi kuelewa njia ila ulikariri jibu. Pepa ilipokuja ukalikuta hilo swali, ukajaribu njia ukakosa 921, ukaamua kubandika njia ya uongo ila Mwishoni ukaweka jibu la ukweli 921. X=921 ukawekewa tiki kubwa(√) na Good ukaonekana kichwa"

NIKASHTUKA Kisha nikasikia; “NOT EVERY BIG RESULT HAD A RIGHT PROCEDURE”. Usiongozwe na upepo ongozwa na Neno. MEASURE EVERYTHING IN THE LIGHT OF THE WORD OF GOD NOT YOUR

FEELING. The wise seek to know the procedure, the fool follows results.

## Kiumbe kipya

Kwa mtiririko huu kuna mambo nilikuwa najiuliza. Sasa, nini kifanyike? Tatizo kubwa lililopo watu wengi waliookoka hawajui wameokoka nini kwa hiyo ni vyema wakafundishwa, kuokoka ni nini? Na kama amekuwa kiumbe kipya huu upya wa maisha una maana gani?

Maana watu wengi wakiwa waumini wa dhehebu fulani wanaandaliwa kuwa waumini wazuri na siyo waamini wazuri na hii imesababisha kuwepo kwa waumini wazuri ambao siyo waamini kabisa; yaani Church Members na siyo Disciples of Jesus.

Changamoto kubwa zaidi ni kwamba hata hao wanaotaka kuwa waumini wanafundishwa vitu ambavyo haviwafanyi wamfananie Kristo Yesu (yaani wanafundishwa kuwafahamu kwa undani wachawi, majini, waganga, n.k)..

Ni lini watamfanania Kristo wakati hawamjui?

Kufahamu kuhusu mambo ambayo Yesu aliyasisitiza na watu waliokaa naye "Mitume" walifundisha kwenye undani kwenye Nyaraka zao. Hizi nyaraka hazipendwi kabisa na watumishi wengi. Changamoto zaidi ni pale Mkristo anafundishwa kuogopa ulimwengu, kuishi kwa hofu na kujitazama kama mtu wa kutendewa mabaya tu (ana maadui, anaibiwa kibali, analogwa, kuna nguvu zinamfuatilia, na

mambo mengine ambayo yanamfanya ajione mnyonge (victim) na mtawaliwa (oppressed) badala ya mtawala (king) na mshindi (winner/victor).

Kristo afunuliwe katika maisha ya watu kwani ndani yake ndiyo kuna uhalisia wote wa uzima wa Mungu...

Yohana 17:3 [3]Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.

Pale mtu anapookoka afundishwe zaidi kuifahamu KWELI.

Hebu jiulize…

Kipi kina nguvu; Mtu kuokoka kwa kuogopa Jehanamu ya moto, au kuvutwa na Upendo usio wa kawaida wa Yesu Kristo? Jibu lako litaamua utahubiri nini ukitaka watu waokoke! Mtu akiingia Nuruni afundishwe kutembea nuruni. Tunatakiwa kufundishwa Noti Original na siyo Fake ikoje! Nimejaribu kukuonyesha, ukombozi halisi ni upi ili siku ukikutana na Fake ujue This is Fake.

Hebu ngoja kidogo tuchambue Waefeso 4:11-15 hapo tutaona kazi ya Mitume, Manabii, Wachungaji, Walimu na Wainjilisti.

Waefeso 4:11 [11]Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; [12]kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; angalia hapo <u>Hata Kazi ya HUDUMA itendeke na ilete matokeo ya ujenzi wa </u>mwili wa Kristo

Waefeso 4:13 [13]hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; Kumfahamu Sana Mwana wa Mungu Hiki ni kitu kikubwa sana Mwana wa Mungu afahamike (Yesu Kristo) si vinginevyo! Watu hata wakifahamishwa juu ya kila kitu duniani na Yesu hawamfahamu ni kujilisha upepo. Hakuna namna unaweza kufika cheo cha utimilifu wa Kristo kama hufundishwi huyo KRISTO mwenyewe! Hatuwezi kujengeka kuwaza na kutenda kama Kristo kama hatufundishwi juu yake! Sasa kufahamu laanza na vifungo na mambo yote bila kumfahamu Yesu Kristo ni kujihakikishia kupotea na kupoteza wengine. Cheo maana yake ni kipimo na kipimo hicho ni Kristo. Yesu Kristo ndiye standards.

Waefeso 4:14 [14]ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za

udanganyifu. Tusipofundishwa juu ya Kristo tunabaki kuwa watoto wachanga hata kama tumeokoka miaka 49 iliyopita kwa sababu hatujakomaa kwa kulishwa juu ya Kristo. Dalili ya kuwa huyu mwanafunzi (disciple) ni mtoto mchanga ni Kuyumbishwa na Mafundisho mapotofu. Atakuwa anakimbia huku na huku kutafuta na kuhangaika kubadilisha makanisa.

Waefeso 4:15 [15]Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Ile kweli juu ya Kristo Yesu ndiyo inayofanya tukue na kumfikia KRISTO sehemu yoyote na katika nafasi yoyote ile. Hakuna mtu atakayesema sasa nimefanana na Kristo ila kila siku tunapofunuliwa zaidi juu ya Kristo ndipo tunapomkaribia zaidi. Huwezi kutengeneza wanafunzi wa Yesu bila kufundisha juu ya Kristo Yesu. Sasa tunavyomfahamu ndivyo tunavyokuwa, ndivyo tunavyomfanania, ndivyo tunapoondoka katika mapooza, ndivyo tunavyoudhihirisha ule ushindi ulioko ndani yetu tayari, ndivyo ule upya unavyoonekana zaidi kama vile dhahabu inavyoondolewa uchafu ili mng'ao wake uonekane kwa uwazi.

## MWISHO

Kufika kwenye ibada zetu na kambi za mafundisho ya neno la Mungu tumia simu +255 714 548 565.
Unaweza kujiunga na vikundi vya mafundisho kwa njia ya mitandao kwa namba hiyo hiyo.

Ukitaka kuwa sehemu ya watu wanaowekeza fedha zao katika kutusaidia kufika injili kwa watu wengine kwa njia ya maandishi na redio tumia +255 763 965 297.

Ku download application yenye mafundisho:
https://play.google.com/store/apps/details?id=com.melayeki
Kuingia katika Website yetu: http://globalfamilygatherings.co.tz
Kuingia channel ya telegram: https://t.me/apostleshemeji
Kuingia Youtube channel:
https://youtube.com/c/shemejimelayeki
Facebook page: https://facebook.com/ShemejiMelayeki
Whatsapp: https://chat.whatsapp.com/JXzsoD5qHlFADN9LdW5Xzo

# UMEBARIKIWA!